# *Sauti ya Ishara*

Asante. Hebu na tuendelee tu kusimama kwa dakika moja, tunaposoma Neno, twende moja kwa moja kwenye Neno usiku wa leo, kusudi tusichukue wakati mwingi sana. Ninataka mfungue pamoja nami, usiku wa leo, kwenye kitabu cha Kutoka, ninii . . . na kuanzia mlango wa 4 wa kitabu cha Kutoka.

> *Musa akajibu akasema, Lakini, tazama, hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu; maana watasema, BWANA hakukutokea.*
>
> *Bwana akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo.*
>
> *Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake.*
>
> *Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake:*
>
> *Ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba BWANA, Mungu wa baba zao, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokea.*
>
> *BWANA akamwambia tena, Sasa tia mkono wako kifuani mwako. Akautia mkono wake kifuani mwake: naye alipoutoa, kumbe! mkono wake ulikuwa una ukoma, umekuwa mweupe kama theluji.*
>
> *Akasema, Tia mkono wako kifuani mwako tena. Akautia mkono wake kifuani mwake tena, na alipoutoa kifuani mwake, kumbe! ume- . . . umerudia hali ya mwili wake.*
>
> *Basi itakuwa, wasipokusadiki, wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.*

2 Na tuinamishe vichwa vyetu. Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu, pia, sijui kama kuna ye yote ndani hapa usiku wa leo aliye na haja ya maombi? Tafadhali ijulikane unapoinua mikono yetu. Mungu na awatimizie haja zenu.

3 Baba yetu wa Mbinguni, tumehesabu jambo hili kuwa ni majaliwa makuu, kuja Kwako katika maombi, tukija katika Jina la Bwana Yesu. Na tumeahidiwa Naye, ya kwamba tukiomba jambo lo lote katika Jina Lake, tutapewa. Wewe unajua haja ya kila mmoja wetu. Unajua kile mikono yetu ilichowakilisha hapo ilipoinuliwa juu. Ninaomba, Baba, ya kwamba utajibu kila ombi usiku wa leo. Jipatie utukufu.

4 Na sasa jalia yule Mwalimu mkuu wa Neno, Roho Mtakatifu, atushukie, usiku huu, na ajifunue kwetu, na—na ajitambulishe kwetu, kwa i—ishara ya kufufuka Kwake. Jalia aje miongoni mwetu, usiku wa leo, Bwana, na—na kuitembelea mioyo yetu. Nena nasi kupitia mambo ambayo ameahidi kwa ajili ya siku hii. Jalia maneno ambayo yameahidiwa kwa ajili ya saa hii yadhihirishwe mbele zetu, ili tuhakikishiwe, katika wakati huu mkuu wa shida ambao Wewe ulisema utakuja juu ya dunia, kuwajaribu watu wote. Na kweli kabisa imefikia wakati huo, Baba, wakati watu wanapojaribiwa. Na kuna pande nyingi mbalimbali, mpaka ni vigumu mtu kujua la kufanya. Lakini, Bwana, ninaomba ya kwamba Wewe utatujulisha, usiku wa leo, ya kwamba uko hapa na uko pamoja nasi, Yuko hapa kutusaidia. Tutimizie haja zetu, kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

5 Nimechelewa kidogo tu kila usiku. Nami wakati wote ninawazia kuhusu maikrofoni *hii*, lakini ni ile iliyounganishwa na vinasasauti. Lakini hii *hapa*, nafikiri, ndiyo ambayo ninayopasa kusikilizia, ama kuzungumzia.

6 Kesho usiku ni usiku wa karamu, kwa hiyo msisahau jambo hilo. Nafikiri ni. . .Nadhani imekwisha kutangazwa, kwamba watu waende wapi.

7 Kwa kweli tunafurahia ushirika wenu katika yale mambo makuu ambayo Bwana wetu amefanya.

8 Sasa, usiku wa leo, ninafikiri ya kwamba, kama hatujui Neno la Mungu, hatujui la kufanya. Hatuwezi kuwa na imani mpaka tujue mapenzi ya Mungu ni nini. Na, vipi, ndipo kama tukijua ni mapenzi ya Mungu, Neno la Mungu linasema jambo fulani, basi tunaweza kufuata jambo hilo kwa furaha.

9 Sasa kama Bwana Yesu angekuwa akitembea hapa, Yeye Mwenyewe, duniani leo, katika mwili wa kibinadamu, Naye akasema, "Kesho mvua itanyesha, siku nzima," sasa ingekuwa ni rahisi sana kwangu mimi kuchukua mwavuli ninapoondoka asubuhi, kwa sababu Yeye alisema hivyo. Sasa, kama Yeye hakusema jambo hilo, basi sijui nitarajie nini. Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, katika kitu cho chote tufanyacho, tunataka kujua ile saa, wakati tunaoishi.

10 Na kwa wageni, juma hili tumejaribu kuonesha ya kwamba Mungu, tangu mwanzo, alijua mwisho. Hilo linamfanya Yeye asiye na kikomo. Kama Yeye si asiye na kikomo, asiye na kikomo, Yeye si Mungu. Naye hana budi kuwa mwenye nguvu zote, aliyepo kila mahali, mwenye kujua mambo yote, na mwenye nguvu zote, apate kuwa Mungu. Hiyo ni kusema nguvu zote, anajua mambo yote, mahali pote, na—na—na anajua mwisho tangu mwanzo. Kama hajui, basi Yeye si Mungu.

11 Kwa hiyo kwa kweli hakuna kitu kilichotoka mahali pake. Ni sisi. Lakini hakuna katika Neno la Mungu; linaenda tu kama saa ya ukutani. Na wakati saa hiyo inapotimia ya jambo hilo kutukia, Neno hilo ambalo limepangiwa wakati huo, linatukia. Huenda tukafikiri linaenda . . . halitatukia. Wakati mwingine linatukia nasi hatujui. Yesu alisema, wakati mmoja . . .

12 Watu walimwambia, "Kwa nini ni—ninii . . . waandishi wote wanasema ya kwamba 'Eliya hana budi kuja kwanza'?" Unaona, sasa, waliamini jambo hilo. Waliamini ya kwamba Eliya alikuwa aje.

13 Naye Yesu akawaangalia, na kusema, "Eliya amekwisha kuja tayari, nanyi hamkujua." Unaona? Sasa, unaona, lilipita papo hapo walipokuwa hao waandishi, wahudumu, wanafunzi. Na ilikuwa ni Yohana Mbatizaji, naye alikuja katika kila njia ambayo huyo Eliya alipaswa kuja, hata hivyo hawakumtambua.

14 Na sasa inatupasa kutambua saa tunayoishi, na wakati tunaoishi. Kutokana na jambo hilo, ninataka kuzungumza usiku wa leo juu ya: *Sauti ya Ishara*.

15 Ni somo geni, hata hivyo Mungu hufanya mambo ya ajabu katika njia zisizo za kawaida. Hilo ndilo linalomfanya Mungu, kwa sababu Yeye ni—Yeye ni wa mbinguni. Katika kila kitu afanyacho, Yeye—Yeye hukifanya. Anaweza kukifanya kimbinguni, kwa kuwa Yeye ni wa mbinguni.

16 Sasa, *Sauti ya Ishara*. Na ni ninii . . . Kuna sauti kwenye ishara. Kuna sauti kwenye damu. Damu ilinena kutoka ardhini, na—na kadhalika, "Damu yenye haki ya Habili ilinena dhidi ya Kaini." Nayo Biblia ilisema, "Damu *ya* Yesu Kristo inanena mambo makuu zaidi kuliko damu ya Habili ilivyonena."

17 Sasa mwelekeo wetu usiku wa leo, ama jukwaa letu, linaanzia katika Kutoka. Na wakati wa Kutoka ni wakati wa kuitwa watoke, na huko kutoka kulikuwa kumewadia.

18 Musa, mtumishi wa Bwana, alikuwa ameitwa hu—hudumani. Na alikuwa anafanya yale aliyowazia, yeye alipata elimu ya juu sana huko Misri, amefunzwa he—hekima yote ya Wamisri, na ilionekana alikuwa na nji—njia, kwamba akiwa mwanajeshi mkuu mwenye kipaji, hivi kwamba angeweza kuwakomboa watu wake kutoka chini ya utumwa huo, kwa kuwa alikuwa Farao-mrithi. Na jinsi ambavyo ingekuwa rahisi kwake kufanya jambo hilo. Lakini, unaona, kama hivyo ndivyo ingekuwa, basi lingekuwa ni jambo la kawaida.

19 Mungu hachukui mambo ya kawaida. Yeye huchukua mambo ya kimbinguni kujithibitisha.

20 Kwa hiyo kutoka katika miaka arobaini ya elimu, ya juu sana ambayo angaliweza kupata, na iliyo nzuri sana angaliweza kupata, msomi hodari sana wa kisomo alivyoweza kuwa; akiwa na ujuzi kutoka kwa mama yake, mwalimu wake, ya kwamba

alikuwa ndiye atakayewakomboa watu hao; ndipo akatoka akaenda katika nguvu za ufahamu wake, na kumwua Mmisri. Na, kutokana na jambo hilo, tunaona ya kwamba jitihada zake zilishindwa, ndipo akakimbilia jangwani.

21 Na kile Misri, katika elimu, ilichoingiza ndani yake katika miaka arobaini, kilimchukua Mungu miaka mingine arobaini kukitoa ndani yake, unaona, kusudi asije akatumainia maadili yake ya elimu. Angetumainia mambo ya kimbinguni.

22 Na sasa wakati ulikuwa umewadia ambao Mungu alikuwa ameahidi, kwa Ibrahimu, miaka mia nne kabla ya wakati huo, ya kwamba uzao wake utakuwa mgeni katika nchi ya kigeni, nao watatolewa. Baada ya miaka arobaini, wangetolewa kwa mkono wenye nguvu. Yeye angewakomboa watu wake kwa mkono wenye nguvu. Na wakati wa ile ahadi ulipokaribia, hapo ndipo Mungu alipomweka Musa jukwaani. Musa, katika kushindwa kwake kabisa, alikuwa ameenda zake jangwani.

23 Sasa mfano hapa, pana mfano wa ajabu ambao bila shaka hatutaki kuukosa. Unaona? Mfano, Mungu alikuwa akiwatoa Israeli, watu Wake, watoke, taifa, taifa moja kutoka katika taifa lingine. Taifa moja kutoka katika taifa lingine, mfano mzuri wa siku hizi, ambapo Mungu anamwita Bibi-arusi Wake kutoka katika kanisa, Bibi-arusi wa Kikristo kutoka katika kanisa la Kikristo, Kanisa Bibi-arusi kutoka katika kanisa, ambalo linaitwa, katika Biblia, linavyotajwa.

24 Nina maandishi mengi na Maandiko yaliyoandikwa hapa, juu ya somo hili usiku wa leo.

25 Linaitwa, mara nyingi, "Waliochaguliwa, Wateule, ama Masalia ya uzao wa mwanamke." Liliitwa, "Bibi-arusi," vile Mungu, kwa kutangulia kujua Kwake, alivyowachagua wawe. Hiyo ni kusema, Bibi-arusi anatoka katika kanisa. Unaona, jambo lote ni kanisa, lakini Mungu huwachukua watu fulani kutoka katika kanisa hilo, kama Bibi-arusi. Yeye alisema angefanya jambo hilo. Naye alilifanya, angalia, ama atalifanya.

26 Angalia, angalia jinsi alivyofanya jambo hilo, na mtindo na jinsi alivyofanya jambo hilo. Tunataka kuangalia jambo hili sasa, alipokuwa akiwatoa Israeli, jinsi alivyofanya jambo hilo, na mbinu alizo—alizotumia.

27 Angalia wakati wa majira ya Neno lililoahidiwa yalipokuwa yatimie, Mungu alimwita Musa, kwa kuchaguliwa tangu zamani, na akamteua kwa ajili ya kazi hiyo. Unaona? Mungu daima amekuwa na mtu aliyewekwa tayari, kwa wakati huo. Hakuna kinachoshindwa kwa Mungu. Yeye amelinena; haliwezi likashindwa. Kama likishindwa, basi Mungu anashindwa, maana Mungu ni Neno.

28 Angalia, sasa, ililipasa Neno lidhihirishwe. Na ilipobidi Neno kudhihirishwa, la ahadi, Mungu daima humtuma nabii

kudhihirisha ahadi hiyo, kwa sababu Neno la Bwana humjia yeye.

29 Musa, aliyechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya kusudi hilo, aliitwa hudumani. Hakuna mtu mwingine ye yote angaliweza kuifanya.

30 Wakati Mungu ame—amekwisha kumwita mtu kufanya kazi fulani, hakuna mtu ye yote anayeweza kuchukua mahali pake. Hakuna mtu anayeweza kuchukua mahali pako, upekee wako.

31 Ni mara nyingi jinsi gani nimeshangaa, jinsi ningetaka kuchukua mahali pa Oral Roberts, jinsi ningetaka kuchukua mahali pa Billy Graham, mtu fulani kama huyo. Kama Billy Graham, niende nikazungumze na kusanyiko la watu, niite wenye dhambi madhabahuni; nisahau jambo hilo na niondoke niende nyumbani, isinilazimu kusimama hapo na kushindana mweleka tena. Mimi siwezi kuwa Billy Graham, lakini wala Billy Graham hawezi kuwa mimi. Sisi wote . . . Siwezi kuwa Oral Roberts; Oral Roberts hawezi kuwa mimi.

32 Ninyi ni, kila mmoja, mmewekwa katika uchumi wa Mungu, barabara kabisa kwa mahali pake. Mtu mmoja hufunga wakati wote na kuzungumza na Mungu, wakati huyo mwingine hutoa pepo kwa sababu huyu anafunga. Lakini ni mwili mzima wa Kristo ukifanya kazi pamoja, umoja. Tunapoona vizuizi hivi vya kimadhehebu vikitutenganisha, hilo ndilo linalouvunja moyo wangu, unaona, kwa maana hicho ndicho kitu kinachotutenganisha. Sisi ni kitu kimoja.

33 Hakuna watu wakubwa kati yetu, hakuna watu wakuu kati yetu. Sisi sote ni sawa. Sisi ni watoto wa Mungu. Kuna mmoja tu aliye mkuu miongoni mwetu, na huyo ni Kristo. Hatuna budi kumtambua. Na kama tukitafuta kupewa heshima, mtu mmoja kwa mwingine, hatuwezi kuwa na imani, kwa maana tunakuwa na imani juu ya sisi kwa sisi. Yatubidi tuwe na imani kwa Kristo. Huyo ndiye Mmoja kati yetu tunayepaswa kuwa na imani Kwake, na kisha imani katika yale anayofanya na yale aliyotupa.

34 Sasa hakuna mtu angaliweza kuchukua mahali pa Musa. Haidhuru alikimbia jinsi gani, na haidhuru alijaribu jinsi gani kulikwepa jambo hilo, walakini Mungu anajua yale anayofanya. Alijua barabara yale hasa aliyotaka kuchukua na kufanya na Musa. Mambo haya yalipaswa yatukie. Sasa, angalia, hakuna mtu angaliweza kupachukua mahali pake.

35 Sasa angalia. Mungu alimpa ishara, kuthibitisha wito wake na madai yake, aliposhuka kwenda Misri.

36 Sasa, Mungu daima humpa mjumbe ishara, na sauti ya hiyo ishara. Na ishara hiyo humtambulisha mtu huyo, kama imeandikwa katika Maandiko.

37 Kama vile Yohana alivyosema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani."

Wakasema, “Je! wewe ni Masihi?”

38 Akasema, “Mimi si Masihi. Bali mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, kama vile nabii Isaya alivyosema.” Yeye aliweza kujitambulisha Mwenyewe dhahiri.

39 Na sasa, basi, kuhusu jambo hilo, tunaona ya kwamba Mungu, daima, habadilishi kamwe njia Yake ya kufanya jambo lo lote. Hawezi kubadilika. Mungu hufanya kila kitu kwa njia ile ile kabisa, wakati Yeye—Yeye anapoweka mfumo Wake pamoja.

40 Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, Yeye alifanya uamuzi mmoja, mwanadamu anapaswa kuokolewa kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia. Tumejaribu vitu vingine vyote, vya kumfanya mwanadamu aokolewe. Tulijaribu kumfikisha mahali ambapo tulijenga jiji fulani, Nebukadreza alijenga jiji. Nao wakajenga mnara, Nimrod alijenga mnara. Wao walikuwa na sheria. Nao wamekuwa na mahekalu. Wamekuwa na makanisa. Wamekuwa na madhehebu. Wamekuwa na mifumo ya elimu, mifumo ya kimadhehebu, wakijaribu kumfikisha mwanadamu kwa Mungu. Jambo hilo, kila kipengele, lilishindwa. Sikuzote litashindwa. Linarudi nyuma moja kwa moja kwenye Damu iliyomwagika!

41 Njia ya Mungu ya kufanya jambo lo lote imenenwa katika Neno Lake. Na Neno hili ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo, hakuna kinachopaswa kuongezwa Kwake wala kuondolewa Kwake. ”Mtu afanyaye jambo hilo,” Biblia ilisema, “ataondolewa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo,” kama akiongeza cho chote ama akiondoa cho chote kutoka Kwake. Lichukue tu jinsi lilivyoandikwa.

42 Biblia haihitaji mtu ye yote kuifasiri. Mungu ndiye anayejifasiria Mwenyewe. Yeye hulifasiri kwa kufanya analosema litimie. Hilo linatosha. Kama Mungu alisema jambo hilo, na akalifanya, imekwisha. Halihitaji mtu wa kulifasiri. Biblia ilisema, “Si ya kufasiriwa kama apendavyo mtu binafsi.”

43 Njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo! Daima akiwa ni mwaminifu kwa ishara yake aliyotuma, Yeye alifuata kwa sauti Yake; kila, tangu, ambapo Mungu anatuma ishara fulani duniani. “Sasa Mungu kamwe hatendi kitu,” Biblia ilisema, “mpaka kwanza Yeye awaoneshe watumishi Wake manabii.” Sasa hilo, wewe. . .kama hilo ni kosa, basi hayo mengine ni makosa, unaona. Yeye hatendi jambo lo lote kamwe mpaka alioneshe.

44 Na huyo mwonaji, nabii, hana budi kutambulishwa, kwamba yale anayotabiri, tunaona katika Hesabu 12:6, ya kwamba yale Yeye anayosema huja kutimia. Basi, amini hilo. Lakini kama hayatimii, basi usiamini. Na haina budi kuwa kwa jambo hilo, ninii Yake. . .haidhuru anene vipi, na linatimia, na cho chote kile; kama jambo hilo halilingani na Neno, basi bado itakuwa ni

uongo. Halina budi kulingana na Neno. Halina budi kuambatana na Neno kwa hiyo ishara ya wakati huo, wakati ambao wanaishi.

45 Sasa, hili lilikuwa limeahidiwa na Mungu, ya kwamba yeye angewakomboa watu Wake kwa mkono wenye nguvu. Sasa, wakati Neno hili, Yeye hakumwita kasisi, Yeye hakumwita rabi fulani, Yeye hakumwita afisa fulani mtendaji. Alimwita mchungaji, kutoka mlimani, mtu aliyezaliwa akiwa nabii, mkimbizi, aliyechaguliwa tangu zamani ambaye hakutaka kazi yake.

46 Unapowasikia watu wakitamani kuwa *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*, kitu fulani, wewe angalia tu, Mungu kamwe hawatumii. Ilibidi Mungu amsake Musa, ili ampate. Ilimbidi kumsaka Paulo, ili ampate. Yeye. . .Ni yule mtu asiyetaka kulifanya, wao hawataki mambo hayo; ndipo Mungu huchukua mtu huyo, ambaye hataki kufanya, kusudi apate kuonesha utukufu Wake kwa jambo hilo.

47 Sasa angalia. Kila—kila ishara ya kweli iliyotumwa na Mungu hufuatwa na sauti. Sasa unaona hapa, somo lenyewe ni. . .ishara na sauti. "Kama hawataamini sauti ya ishara ya kwanza, basi wataamini sauti ya ishara ya pili." Sasa, ishara ina sauti. Na, sasa, kila ishara ya kweli iliyotumwa na Mungu ina sauti, na sauti hiyo haina budi kuzungumza kulingana na Neno lililotolewa kwa ajili ya wakati huo, barabara kabisa.

48 Kama sauti ikija, sauti ile ile ya kale ya ninii ile ile ya kale. . .Ukiona ishara, hasa, na ishara hiyo ambayo mtu huyo anafanya ni itikadi ile ile ya kale ya mawazo, basi unaweza kusema mara moja, "Hiyo haikutoka kwa Mungu," kama inaendelea kutambulisha itikadi ile ile ya kale ya mawazo. Kamwe haikutoka Kwake. Haijatoka Kwake kamwe. Ingekuwa ni kinyume cha utaratibu wa Mungu.

49 Haina budi kuwa ni kitu fulani kipya. Haina budi kuwa ni kitu fulani ambacho watu hawafahamu. Haina budi kuwa . . . la sivyo haingetumwa. Haipaswi kutumwa, kama ni shule ile ile ya kale ya theolojia. Haina budi kuwa ni jambo fulani tofauti, hata hivyo haina budi kutambulishwa katika Neno, ya kwamba hiyo ni ya siku hiyo. Unaona, uhalisi wa Neno la Mungu, haina budi kuwa hivyo. Hakuna makosa kwake. Haina budi kuwa ni Kweli; haina budi kuthibitishwa na Mungu, kwamba ni Kweli. Na mtu anayelinena hana budi kuthibitishwa na Mungu, kwamba ni mwonaji kutoka kwa Mungu, la sivyo ni makosa; wao hata—hata hawalioni, hata kidogo, hata hawaliamini.

50 Ishara zi—zinatoka kwa Mungu. Ishara inayofuata. . .Ama, sauti inayofuata hiyo ishara haina budi kuwa ni sauti ya Mungu ikinena kutoka kwa Neno, kwa ajili ya wakati huo. Je! mnaelewa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

51 Mungu hutoa ishara. Yeye anafanya hivyo kwa ajili gani? Daima hutoa ishara! Yeye aliwaambia watamtafuta Yeye katika

hizo, hizo ishara. Mungu hutoa ishara apate kuvuta usikivu wa watu Wake. Sasa hebu na tusome jambo hili, kindani. Unaona, ishara zinatolewa kuvutia usikivu wa watu. Kwa sababu, ishara iliyotumwa na Mungu inapotolewa, Mungu yuko tayari kunena. Mungu yuko tayari kunena, wakati ishara imetolewa. Kama inatoka Mbinguni, inatoka kwa Mungu, na Mungu yuko tayari kuzungumza na anajaribu kuvuta usikivu wa watu.

52 Na Neno humjia nabii Wake. Naye nabii anatambulishwa na ishara ambayo anaonesha, halafu anakuja kwenye Neno nalo Neno linadhihirishwa. Hilo linatosha; halihitaji fasiri yo yote. Mungu amelifasiri tayari. Unaona, ni kamilifu tu kama iwezavyo kuwa.

53 Sasa angalia, Mungu hutoa ishara kuvutia usikivu wa watu.

54 Hapa, kijiti kilichowaka moto kilikuwa ni ishara ya kumvutia yule nabii; kile kijiti kilichowaka moto. Musa alikuwa, nyuma ya jangwa, akiwachunga kondoo wake, mzee mchungaji, miaka themanini, ndevu ndefu; akienda zake, akishuka kwenda kwenye njia ndogo ya kale aliyoizoea, kwenye asubuhi yenye joto, labda. Halafu basi, mara, kukatokea kijiti kilichowaka Moto, na kijiti hicho hakikuteketea. Vema, hilo lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida kabisa.

55 Sasa, Musa akiwa ni mwanasayansi, ambapo, yeye alifundishwa katika hekima yote ya Wamisri, nao walikuwa wanasayansi wakuu zaidi kuliko tulio nao siku hizi; kwa hiyo kwa kuwa alikuwa mwanasayansi, ilionekana kana kwamba angalisema, "Sasa nitaenda nione ni ninii za aina gani . . . za kemikali zilizonyunyiziwa yale majani, hata mti huo hauteketei." Unaona, kama yeye angelifuatilia jambo hilo katika njia ya kisayansi, kamwe haingezungumza naye.

56 Na ndivyo ilivyo siku hizi, wakati tunapojaribu kuliendea kupitia shule na elimu, katika njia ya kisayansi, utamkosa Mungu maili milioni moja. Liendee kama Musa, akiwa amevua viatu vyake; mnyenyekevu, unyenyekevu.

57 Na, sasa, palikuwo na ishara ya kumvutia nabii. Sasa, pale, ishara hiyo haina budi kuwa na sauti. Na wakati sauti hiyo iliponena, kama isingalikuwa ya Kimaandiko, siamini huyo nabii angaliisikiliza. Lakini angalia jinsi sauti hiyo iliyoambatana na hiyo ishara ilivyokuwa ya Kimaandiko, ilithibitisha ilikuwa ni Mungu, kwa kuwa Yeye alisema, "Nimesikia kuugua kwa watu Wangu, Nami ninakumbuka ahadi niliyowaahidi." Unaona, ile ishara, kisha sauti ya Kimaandiko nyuma ya ishara hiyo.

58 Sasa hiyo inaonesha kabisa yale niliyoweka msingi hivi sasa tu. Haina budi kuwa ni ishara kutoka kwa Mungu, na, kama ndiyo, kuna sauti ya Kimaandiko nyuma yake, kwa ajili ya ahadi ya siku hiyo. Si itikadi ile ile ya kale; waalimu na kadhalika waliokuwa wakipitia kwenye shule hizo, ama kila kitu, sikuzote,

sikuzote, makasisi, na kadhalika. Lakini hiki ni kitu kipya, ni cha Kimaandiko, ni ahadi; na ishara ya kumvutia nabii.

59 Na basi, Yeye akasema sasa, kabla ya yeye kushuka kwenda kule chini, hana budi kuwa na kitu cha kujithibitisha mwenyewe kuwa nabii, unaona, kabla ya wao kumpokea. Kasema, "Wao hawatasema Bwana amenitokea."

60 Kasema, "Basi, nitakupa ishara mbili za kufanya, na hizo zitavutia usikivu wa watu. Na usikivu wa watu utakapovutiwa, basi nena maneno haya kwao, 'Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, Nami ninakumbuka ahadi Yangu.' Nami nimekutuma huko ukawakomboe, nami nitakuwa pamoja nawe."

61 Je! uliiona ishara yake ya kwanza? Yeye alikuwa na kila namna ya waigaji wa hizo. Kila mtu alijaribu kutupa nyoka chini. Hiyo ni . . . Kama hiyo si tabia ya watu, mimi sijui nyingine, unaona. Unaona? Lakini wao walikuwa na sauti ya aina gani nyuma ya hiyo? Hakuna; sauti ya ulimwengu ya Wamisri. Hata hivyo wao wangeweza kufanya ishara, bali hawakuwa na sauti nyuma yake, kuiunga mkono. Lakini Musa alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ndiyo ilikuwa tofauti yake. Waigaji hatimaye waliendelea kwa muda mrefu, lakini hatimaye waliishiwa.

62 Je! unajua Biblia ilisema jambo hilo lingetukia tena katika siku za mwisho? "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo na watu walioharibikiwa na akili zao kuhusu ile Kweli." Kweli ni Nani? Yesu Kristo ndiye Kweli. Unaona? "Walioharibikiwa na akili zao kuhusu ile Kweli."

63 Sasa Yehova yuaenda kunena kwa Neno Lake lililoahidiwa. Hana budi sasa kumtayarisha nabii huyu apate kumtuma. Kwa sababu, ndivyo yalivyo mawazo Yake daima, njia Yake ya kutenda kazi, sikuzote humtuma nabii Wake akiwa na Neno, na anamthibitisha nabii huyo.

64 Tena, hii ni ishara iliyoahidiwa. Nabii, mwenyewe, ni ishara. Biblia ilisema hivyo. Unapoona nyakati zikipita, na halafu uone akija . . . Chukua historia ya Biblia, uisome. Kila unapoona kipindi kirefu cha wakati kimepita; lakini mara unapoona nabii akitokea, ilikuwa ni ishara ya hukumu. Mungu alikuwa akitaka kuuhukumu ulimwengu, wakati Yeye . . . ama taifa, ama watu, ulipoona nabii akija. Nimehubiri mahubiri juu yake, ninyi watu wa kanda mnakumbuka, ninii . . . *Ishara ya Kweli Iliyopuuzwa*. Kila wakati wanaipuuza, sikuzote wameipuuza, lakini ilikuwa ni ishara ya hukumu ijayo.

65 Sasa Neno Lake linatimizwa katika sauti Yake. Yale anayoahidi, ndipo anatimiza Neno Lake kwa sauti.

66 Kuja kwa nabii ni ishara ya kuonya ya kwamba hukumu imekaribia. Imekuwa hivyo daima. Hebu ninukuu tu moja.

67 Angalia Nuhu akiinuka katika ninii za mwisho, katika—katika siku zile zilizotangulia ile gharika, nabii akitabiri. Ilikuwa ni kitu gani? Hukumu ilishuka mara tu baada ya hayo.

68 Musa alienda Misri, nabii aliyethibitishwa kwa ishara za nabii. Ni jambo gani lililotukia? Hukumu iliipiga Misri mara tu baadaye.

69 Eliya akajitokeza jukwaani, nabii, na kumtabiria Ahabu na taifa hilo. Nini kilitukia? Hukumu ilishuka mara baada ya hayo. Kweli.

70 Yohana Mbatizaji akajitokeza, kama ishara. Yeye alikuwa ni nabii. Alikuwa ni ishara ya nabii aliyekuja duniani. Wao walijua, wakati alipojitokeza, Masihi angenena, baada yake. Ilibidi iwe hivyo, maana, kuwapata—kuwapata wateule.

71 Kusudi la jambo hili ni kuwapata watu walioteuliwa wanaotoka, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Kama ilivyokuwa katika siku za—za Eliya, wale elfu saba ama mia saba, ama wo wote wale, ambao hawakuwa wamepigia goti, kuwaita watoke. Yohana akiwaita wateule, na kuwakabidhi kwa Kristo wakati Yeye alipokuja, akabadilisha kanisa lake, kasema, "Sina budi kupungua, Yeye hana budi kuongezeka, kwa sababu," alisema, "mimi ni sauti Yake tu, iliayo nyikani, 'itengenezeni njia ya Bwana.'" Naye Yesu alikuja namna ile ile. Inawafanya wateule tayari kuisikia sauti ya Mungu, hilo ndilo kusudi la ishara ya kinabii. Loo, kama ukizifuata jumbe hizi, kuwafanya ninii . . . kuwafanya wateule wawe tayari. Si hao wengine, kamwe hawataisikia. Wateule ndio wanaoitwa.

72 Yule Malaika alikuja wapi, Sodoma, yule aliyefanya ile ishara? Kwa Ibrahimu pamoja na kundi lake. "Usiukaribie Sodoma; utateketezwa!" Unaona? Yesu aliahidi jambo hilo kujirudia, mnajua, tena, katika Sodoma hii. Sasa angalia.

73 Inafanya nini? Inawafanya wateule wawe tayari kwa ajili ya mahali pa kimbilio la Mungu, kama ilivyokuwa katika wakati wa Nuhu, na kadhalika.

74 Nayo inafanya nini? Inamhukumu yule msomi asiyeamini, kumtia hukumuni. Sikuzote inamhukumu. Kukataa rehema, hakuna kilichosalia ila hukumu. Kwa hiyo inamweka—inamweka msomi na yule asiyeamini tayari kwa ajili ya hukumu. Kwa sababu, wao wanafanya nini? Wanaikataa.

75 Hiyo ndiyo sababu Wayahudi walikula nyama za miili yao wenyewe. Hiyo ndiyo sababu damu ilitiririkia nje ya mji wakati Tito, yule jemadari mkuu wa Kirumi, alipoingia mle, ni kwa sababu walikuwa wamemkataa Roho Mtakatifu. Ilibidi hukumu ije kwa sababu walikuwa wamemdhihaki. Yesu aliwaambia, wakati walipomwita Beelzebuli, kwamba alisema, "Ninawasamehe," upatanisho haukuwa umefanywa, "lakini," kasema, "wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo

lile lile, kusema neno dhidi Yake hakutasamehewa kamwe." Na kizazi hicho hakikusamehewa jambo hilo kamwe. Hiyo ni kweli.

76 Hukumu kwa asiyeamini! Inawekwa huko nje kwa kusudi hilo, kumpa mwamini nuru, na giza kwa asiyeamini. Kama tu vile ile nguzo ya Moto ilivyokuwa; ilitoa nuru, kuvuka kuingia kwenye nchi ya ahadi, na giza kwa wale ambao hawakuamini. Ishara za Mungu daima hufanya hivyo, hupofusha macho ya asiyeamini, na kumpa mwamini kuona na nuru ya kutembea. Hiyo ndiyo sababu ya kutumwa Kwake.

77 Kama unabii wake ni wa kweli, kama unabii wa nabii ni wa kweli na unatimia, basi ni onyo la Mungu. Sasa katika Hesabu 12:6, tunaona jambo lile lile, Maandiko.

78 Biblia iliandikwa na watu hawa. Sasa kama tukisoma katika Petro wa Pili 1:21, ilisema, "Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Biblia."

79 Pia katika Waebrania 1:1, ambapo tulizungumzia hivi majuzi usiku, "Mungu, kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alisema na baba zetu katika manabii, siku hizi za mwisho katika Yesu Kristo, Mwanawe."

80 Ile Nguzo ya Moto, hiyo ishara; sauti . . . ama sa—sauti ile ilikuwa inene. Ile Nguzo ya Moto katika kijiti, ilikuwa ni sauti maalum kwamba Mungu alikuwa yu karibu kunena.

81 Angalia kwa makini sasa, usikose jambo hili. Wakati Miriamu alipokuwa amemcheka ndugu yake, Musa, naye alikuwa ni nabii mke wakati alipomcheka, naye Mungu akashuka katika Nguzo hiyo ya Moto, Musa alijua ya kwamba Mungu alikuwa tayari kunena. Ilikuwa ni ishara. Na sauti iliyoifuata, ilisema, "Je! hamumwogopi Mungu?" Kasema, "Hakuna mtu nchini kama mtumishi Wangu, Musa."

82 Alifanya jambo lile lile wakati walipoinuka na kusema kuna ninii . . . Wakati Dathani alipoinuka, na wakati Kora, maasi yake, "Kuna watu wengi watakatifu kuliko wewe. Unafikiri wewe ndiwe pekee katika kundi hili." Mungu alikuwa amemchagua Musa kufanya kazi hiyo!

83 Na wakati walipotaka kupata kundi lingine liambatane nao, wajifanyie madhehebu, Akasema, "Jitenge nao. Nitawahukumu tu. Nitawaangamiza tu," Naye aliwaangamiza. Ulimwengu ukawapata.

84 Sasa tunaona ya kwamba sikuzote hiyo imekuwa ndiyo njia ya Mungu. Nguzo ya Moto inaonesha Sauti inataka kunena. Loo, kamata jambo hili! Mnaweza kuwa vipofu jinsi gani? Mngali mnakumbuka Houston. Sasa kuna Sauti inayofuata ile ishara.

85 Musa, ishara ya nabii kwa Israeli, aliahidi ya kwamba Neno liko tayari kuthibitishwa.

86 Jinsi Neno la Mungu lilivyo kamilifu, katika utaratibu, kila wakati! Ni kama tu Urimu Thumimu, kama nilivyosema, usiku

wa juzi. Urimu Thumimu zilikuwako, na isipokuwa hiyo ishara ije kwenye Urimu Thumimu hizo, hiyo sauti haikukubaliwa. Hapana budi kuwe na ishara. Ishara inathibitisha sauti. Na sauti inathibitisha ishara, kwamba inatoka kwa Mungu. Sauti ya ishara ndiyo inayosema "ndiyo" ama "siyo." Kama Mungu aliikataa, basi hiyo Sauti inasema "la." Kama ishara ilikuwako, Mungu alisema "ndiyo." Utaratibu wa Mungu haujabadilika hata. Tungeweza kukaa saa kadha kwenye jambo hilo, bali kamwe haujabadilika.

87 Angalia, nabii Yona, angalia ile ishara. Yeye alikuwa akienda zake Tarso. Akaanza kwenda Ninawi, na akashika nji—njia ya kwenda Tarso. Wengi walimlaumu Yona. Yona hastahili kulaumiwa. Yeye alikuwa nabii. "Hatua za mwenye haki zinaongozwa na Bwana," naye akaanza kwenda zake Tarso. Nasi tunajaribu kumlaumu mtu huyo, bali Yesu hakumlaumu.

88 Angalia, Yeye alisema, "Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku," ilikuwa iwe ishara, "vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi, siku tatu mchana na usiku. Na kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara, wala hakuna ishara itakayotolewa kwao kutoka kwa Mungu, kumbukeni, ila ishara ya Yona." Ishara ya Yona ni nini? Ufufuo. Na hiki ni kile kizazi cha Sodoma, kizinzi, uzinzi wa kiroho, wa-. . . wakifanya uzinzi wa kiroho dhidi ya Kweli ya Mungu, wakiifanyia mzaha. "Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara, nao wataipata, itakuwa ni ishara ya ufufuo." Angalia, Yona . . .

89 Hao watu walikuwa ni makafiri, na ilikuwa ninii kubwa . . . Ulikuwa ni mji wa kibiashara. Biashara kuu ilikuwa ya samaki. Walipeleka samaki kote nchini. Hao watu walikuwa ni wavuvi. Hiyo ndiyo iliyokuwa kazi yao. Nao walikuwa ni makafiri, waliabudu wanyama na sanamu, nao wakawa waovu sana.

90 Ni kama vile taifa hili sasa, lililojaa zinaa na Hollywood, na kila namna, hata ndani ya makanisa. Basi angalia linalotukia. Mbona, mara nyingi hata tamaa ya zinaa kanisani inasemekana kwamba ni jambo la kisasa. Taifa hili linawezaje kusimama chini ya upuuzi kama huo? Kujiita Wakristo, na kufanya mambo kama hayo, linawezaje kusimama?

91 Kama vile rafiki yangu wa thamani, Jack Moore, alivyosema, miaka mingi iliyopita, "Kama Mungu akiliacha taifa hili likubalike kwa jambo hili, Yeye atawajibika, kama Mungu mwenye haki, kuinua Sodoma na Gomora, na kuwaomba msamaha kwa kuwatetekeza kwa moto."

92 Lazima mhukumiwe. Hakuna njia nyingine ya kutamka jambo hilo kwa dhati. Liandikeni hilo katika Biblia zenu. Ninakuwa mzee. Mwone kama halitahukumiwa. Kama nikiishi maisha ya kawaida, nitaona jambo hilo, umri wa kawaida. Miaka mingine michache italifikia jambo hilo.

93 Yona. Wote walikuwa wametoka kwenda kuvua samaki, yapata majira ya alasiri, na huyu hapa mungu wa bahari anakuja, anatokeza juu, yule nyangumi, akakimbia ukingoni na kumtema nabii ukingoni. Jamani ni ishara ya jinsi gani!

94 Mungu alimleta nabii Wake, akiwa na ujumbe. Sasa wao waliiona hiyo ishara, wakaamini hiyo ishara, sasa ujumbe ni nini? "Tubuni!" Hiyo ndiyo sauti ya ishara hiyo. Sauti ya ishara hiyo ni, "Tubuni, la sivyo kabla ya siku arobaini mtaangamizwa." Wao waling'amua wapaswayo kutubu.

95 Yesu alisema, "Watakihukumu kizazi hiki, maana walitubu kwa mahubiri ya Yona; aliye mkuu kuliko Yona yupo hapa."

96 Ile sauti ilikuwa, "Tubuni, la sivyo kabla ya siku arobaini mtateketezwa."

97 Yohana yule nabii, akitokea, ishara ya kutokea kwa nabii, baada ya miaka mia nne bila nabii. Walikwisha kuwa na watu wote wenye akili. Ninawazia tu mchafuko waliokuwa nao! Miaka mia nne, bila nabii, lakini wakati ulikaribia ambao Masihi alipaswa aje. Sasa, Yohana alikuwa ni ishara, akiwa nabii, ya kwamba Masihi alikuwa tayari kunena, sauti ya ishara hiyo; kwa sababu, katika Malaki 3, tunaona, "Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu." Ilibidi Eliya aje mbele ya uso Wake, na Eliya akaja. Yohana, katika roho na nguvu za Eliya, alikuja na kufanya yale Maandiko yalichotimiza hasa, wala hawakufahamu jambo hilo. Maandiko yanasema hivyo. Yeye alikuwa ndiyo ishara, ishara ya nabii, ya kwamba Masihi atanena.

98 Nabii huyo, alijua vizuri sana jambo hilo, hata akasema, "Mbona, kuna Mtu anayesimama miongoni mwenu, sasa hivi. Huyo Masihi ninayenena habari Zake, yupo miongoni mwenu. Sistahili kufungua viatu vyake. Yeye ndiye atakayewabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto. Mimi nawabatiza kwa maji, kwa toba, lakini Yeye atakuja nyuma yangu. Yeye yuko kati yenu hivi sasa."

99 Siku moja aliona kijana Mwanamume akija, akishuka. Akaona ile Nguzo ya Moto, katika umbo la Hua, ikishuka kutoka Mbinguni; Sauti, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Inasema, "Nipendaye kukaa ndani Yake," ni kitenzi tu mbele ya kielezi, kwa hiyo ni mamoja tu. "Ninayependezwa kukaa ndani yake," ama, "Ambaye ninapendezwa kukaa Kwake," haileti tofauti yo yote. Angalia, "Ninapendezwa kukaa ndani Yake."

100 Yohana alisema, "Ninashuhudia ya kwamba Yeye aliyeniambia huko jangwani," si katika seminari, "jangwani, alisema, 'Yule ambaye utaona Roho akishuka juu Yake, na kukaa juu yake,' amina, 'Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.'Nami nashuhudia kwamba ni Kweli."

101 Ilikuwa ni nini? Nabii huyo alikuwa ni ishara ya kwamba Masihi alikuwa tayari kunena.

102 Masihi alikuwa nini? Masihi alikuwa ni Neno, katika ukamilifu. Yeye alikuwa utimilifu wa Mungu. Manabii walikuwa Nuru ndogo iliyomulika. Lakini ndani Yake mlikuwamo na Nuru hiyo yote, ilikuwa katika Masihi huyu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa, aliyefanywa Imanueli, Mungu miongoni mwetu katika mwili wa kibinadamu.

103 Masihi alikuwa tayari kunena. Basi angalia, Biblia inasema, ya kwamba, "Neno la Bwana huja kwa nabii."

104 Sasa hapa alisimama Yohana, ambaye Yesu alisema alikuwa "nabii mkuu sana kuliko manabii wote waliopata kuishi." Yesu alisema hivyo, Mathayo sura ya 11. "Mlitoka kwenda kuona nini, mtu anayetikiswa na kila upepo, madhehebu *haya* yanasema, 'Nitakuongezea; je! utafanya *hivi*'? Si Yohana! La, la. Mtu ambaye anaweza kusukumwa-sukumwa, kuchukuliwa huku na huko? La, yeye alikuwa ni nabii mkali, asiyembembeleza mtu. Je! mlienda kumwona mtu ambaye alikuwa amevikwa joho la ukuhani?" Kisha akasema, "La, hao wanakaa kwenye majumba ya wafalme. Wanawafungia ndoa vijana, wanabusu watoto wachanga, na kuzika wazee. Ni wa aina hiyo. Hawajui kitu juu ya Upanga ukatao kuwili. Kwa hiyo mlitoka kwenda kuona nini, nabii?" Akasema, "Zaidi ya nabii!" Ni kweli, yeye alikuwa ni mjumbe wa Agano, Mungu aliahidi atamtuma.

105 Basi angalia hapa, Yohana akiwa amesimama majini, akibatiza, akisema, "Yuaja."

106 Na Neno liko hapa, si likiwa tena Mbinguni, bali lililofanyika mwili. Neno ni mwili, inakuwaje basi? Utaratibu wa Maandiko ya Mungu ni upi? Neno lilimjia nabii, moja kwa moja jangwani, moja kwa moja kwenye kile kidimbwi. Neno lilimjia nabii.

107 Yohana akaangalia juu, na akasema, "Mimi ninahitaji kubatizwa na Wewe."

108 Na rafiki yangu mpenzi, ndugu wa siku nyinig, Daktari Davis, kanisa la Kibaptisti la Kimishenari, ambaye alinibatiza katika imani ya Kikristo, kama yeye yuko hapa usiku wa leo, simaanishi kumuudhi. Maana, yeye anaishi hapa Texas, amewasili hapa kutoka Mlima Davis. Lakini ninakumbuka tulipokuwa tukibishana juu ya jambo hilo siku moja, nami nikiwa ni mvulana tu. Basi nikasema, "Haiji, Daktari Davis."

109 Akasema, "Kilichotukia ni kwamba, basi Yesu akambatiza Yohana, halafu naye Yohana akambatiza Yesu, kwa maana Yohana hakuwa amebatizwa." Halikuonekana ni sahihi kwangu.

110 Nikaendelea kungojea, nikiangalia, nikishangaa. Nisingesema neno lo lote juu yake, isipokuwa siku moja wakati Bwana alipolifunua.

111 Sasa angalia vile Yesu alivyosema. Yohana alisema, "Nina haja ya kubatizwa na Wewe, basi mbona unanijia mimi?"

112 Yesu akasema, "Kubali hivi sasa, kwa kuwa imetupasa kutimiza haki yote."

113 Yohana alijua kwamba Huyo alikuwa ni Nani. Hao hapo viongozi wawili wa ulimwengu, viongozi wawili wa kanisa, Mungu na nabii Wake, wakisimama pamoja. Sasa, angalia, walipaswa kujua.

114 Yesu akasema, "Kubali hivi sasa, hilo ni kweli, lakini ndivyo inavyotupasa kwamba tutimize haki yote, Neno lililoahidiwa."

115 Ilipasa Dhabihu kuoshwa kabla haijatolewa. Yohana alimbatiza Yesu kwa maana Yeye alikuwa ndiyo Dhabihu. Unaona? Dhabihu ilipaswa ioshwe kabla haijatolewa. Akatoka moja kwa moja, na hiyo Dhabihu ikawa imeoshwa, halafu ametolewa ipaswavyo. Akasema, "Huyo ndiye yule Mwana-Kondoo wa Mungu."

116 Alienda moja kwa moja ukingoni, na huyu hapa Roho wa Mungu akaja akishuka juu Yake, akasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu." Unaona, hapo ndipo alipotolewa kwa watu. Lakini kabla Dhabihu hiyo kuruhusiwa kutolewa, ilibidi ioshwe kwanza; hiyo ndiyo kanuni ya Agano la Kale. Vema.

117 Masihi alikuwa karibu kunena, kwa maana hapa palikuwa na ishara ya nabii. Na wakati walipomwona nabii huyo akijitokeza jukwaani, baada ya miaka hiyo yote mia nne bila ya kuwa na mmoja, wao walijua, sauti inayofuata ilikuwa ni ya Masihi.

118 Sasa ninyi wasomaji wa Biblia fikirieni kwa makini kwa dakika chache. Walipoangalia tabia yake, aliwapitaje? Walikosaje kujua ya kwamba huyo alikuwa ndiye, yaani Yohana? Tabia yake ilitambulika, roho yake na tabia yake zilitambulika kuwa ni Eliya. Sasa angalia ni roho gani. Sasa, yeye alikuwa ni Yohana Mbatizaji, lakini roho wa Eliya ndiyo ambayo ilikuwa juu yake.

119 Angalia, kwanza, Eliya alikuwa mtu aliyependa nyika. Unaona? Naye Yohana alikuwa ni mtu wa nyikani.

120 Na Eliya alikuwa mtu aliyekemea huo mfumo wa kimadhehebu, katika wakati ule, kwa nguvu zake zote. Vivyo hivyo na Yohana, "Enyi uzao wa nyoka. Ni nani aliyewaonya kuikimbia ile ghadhabu? Msianze kusema, 'Nina *hiki, kile,* ama *kinginecho*.' Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Unaona tabia hizo mbili?

121 Basi mwangalie Eliya, yeye alikemea Mayezebeli wote wenye nyuso zilizopakwa rangi wa siku zake, hao wanawake wazinzi.

Je! Yohana alifanya nini? Jambo lile lile, kwa Herodia. Wote wawili, ilikuwa ndilo jambo lililosababisha kifo chao.

122 Mwangalie Eliya, baada ya kufanya kazi ile kubwa, yeye angeshikwa na moyo wa huzuni, akalala pale na kumwomba Mungu amchukue. Yohana alifanya vile vile, hata alilala pale na kuwatuma wanafunzi wake, kasema, "Nendeni mkamwulize. Je! Yeye Ndiye ama tumtazamie mwingine?" Yesu alijua jambo hilo.

123 Yeye alikuwa ni Eliya. Hayo yalibidi yawe ndiyo maumbile yake. Alitambulishwa hasa kama Eliya kabisa alivyotambulishwa. Alikuwa katika roho ya Eliya.

124 Inapaswa ije mara tano, hiyo roho inapaswa kuja, kutumiwa juu ya Eliya, Elisha, Yohana, na Malaki 4, halafu kwa ajili ya Wayahudi katika siku za mwisho! . . . ? . . . roho ya Eliya! Angalia sasa.

125 Leo, nawatakeni muwaangalie manabii wetu akina Ahabu wa kisasa leo, wakiwaruhusu Mayezebeli wao wakate nywele zao, wapodoe nyuso zao, wavae kaptula, wavute sigara, cho chote kile. "Hakuna neno." Manabii we—wetu akina Ahabu wa leo, wakiendelea na madhehebu yao, hakika, wakiwaongoza huku na huko kwa kanuni za imani na madhehebu ya kujibunia. Ni kitu gani? Manabii wa Ahabu.

126 Tunahitaji Mikaya mwingine ajitokeze jukwaani. Ama katika wakati wa Ahabu, Eliya ajitokeze jukwaani. Huyo ndiye, aliyeahidiwa.

127 Wakiwaongoza kila mahali, vyo vyote vile wanavyotaka kwenda. Kama hawafanyi hivyo, wawasumbue hapa mahali fulani, wataondoka waende wakajiunge na *hili* na bado waendelee kushikilia ushuhuda wa—wa—wao wa Kikristo.

128 Vema, wao hawajawahi kuokolewa kamwe, hapo mwanzo. Tabia yao yenyewe inathibitisha jambo hilo. Je! unaweza kuchuma mabalungi kutoka katika mti wa miiba? Je! unaweza kupata matikiti maji kutoka katika mzabibu wa boga? Tabia yenyewe inaonesha hawalitaki Neno hata kidogo. Wanalidhihaki, na kulikufuru. Ambapo imeandikwa, "BWANA ASEMA HIVI, mambo haya hayana budi kutukia," nao wanalicheka jambo Hilo, wanalidhihaki.

129 Si ajabu Yesu alisema, "Malkia wa Kusini atafufuka pamoja na kizazi hiki, katika siku za mwisho, na kukihukumu; kwa kuwa alitoka pande za mwisho za dunia, ile akmwone mtu mwenye karama ya hekima." Yeye akasema, "Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa." Hakika. Sulemani alikuwa, katika siku zake, ilikuwa moja ya zile siku kuu. Watu wote waliamini karama hii ambayo walipewa na Mungu, huyu Sulemani, na ninii yake—sifa zake zilisambaa kila mahali. Vipi kama sisi watu wa siku hizi . . .

130 Na sisi Wamarekani, daima tunajaribu kupata mbinu dhidi ya ukomunisti. *Huu* hapa mpango wa Mungu, "Tubuni! Mgeukieni Mungu!" Ati mbinu fulani? Kama wangefanya tu jambo Hilo, tungesahau ukomunisti.

131 Wakati Israeli wote walipoamini ile karama ambayo Mungu aliwapa. Laiti Marekani ingalitoa ninii tu... ingaliamini karama ambayo Mungu ametupa, siku hizi za mwisho, Mwanawe, katika umbo la Roho Mtakatifu, aliyefufuka katika wafu, akiishi miongoni mwetu kulingana na ahadi yake. Laiti tungalitunza jambo Hilo kwa upendo!

132 Hilo litaenda tu kwa wateule peke yao. "Kwa kuwa hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watakuja." Ni kupanda mbegu tu; zinaanguka, baadhi yake *hivi* na baadhi yake *hivyo*, lakini kuna kupanda mbegu, hata hivyo. Zote zitashika mizizi yake po pote zilipo. Zitalipokea.

133 Angalia, hawa hapa, nasi tunaona ya kwamba katika siku zile, Ahabu, hilo taifa liliwafanya hao Israeli kutenda lo lote walilotaka kutenda, na bado wakikiri kwamba wao ni Israeli.

134 Jinsi ambavyo Eliya alivyokikemea kizazi hicho, kwa yote yaliyokuwa ndani yake, naye Mungu akimthibitisha. Naye alikuwa ni nabii.

135 Kabla tu ya kule kuja, vivyo hivyo Yohana! Alienda moja kwa moja Israeli...Alikuwa amemwoza mwanamke huyu na—na Hero-...na Herode, mke wa ndugu yake Filipo. Akaenda moja kwa moja mbele zake; hakurudi nyuma. Hakuhofu mzee fulani ati atamfukuza. Hakuwa na kadi ya ushirika; alikuwa tu na Mungu. Yeye alikuwa ni nabii Wake. Alikuwa na Neno. Haikumbidi kwenda kumwuliza askofu ye yote wala mashemasi. Alikuwa ametiwa mafuta. Alikuwa na Neno. Alienda moja kwa moja mbele zake, na kusema, "Si halali kwako kumwoa!" Kweli. Hakutaniana, na mtu ye yote.

Hao wanawake waovu wakifanya uzinzi, wakifanya yasiyofaa!

136 Kama vile Amosi, alipojitokeza jukwaani, aliangalia kule. Hata hatujui alikotoka. Jamani, jinsi hapana budi alivyoangalia jiji hilo la Samaria! Kama vile watalii walivyofanya, jiji zima lilipendeza, na wahubiri wote wameungana na ma—mataifa, na umoja wa mataifa na kila mtu, na hata hivyo wakiishi katika dhambi! Macho yake yakasinyaa, upara wake ukang'aa, na hivyo akashuka akaja. Hakuninii...hakuwa mzuri sana wa kumtazama, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI.

137 Tunahitaji Amosi fulani ajitokeze jukwaani leo. Je! tungempokea? La hasha, si zaidi ya vile alivyofanya. Yeye angejitokeza jukwaani, angerarua kila shirika, kila madhehebu, kila mwanamke anayevaa kaptura, kila Yezebeli aliyekata nywele zake. Angewararua vipande-vipande. Wao

wangemfukuza mtaani, na kusema, "Huyo mzee mshupavu wa dini!" Lakini angekuwa na BWANA ASEMA HIVI, kwa maana imeandikwa hivyo tu. Je! madhehebu yangempokea? La.

138 Hakuwa na mtu wa kudhamini mikutano yake. Je! jiji hili kuu, zuri la—lililojaa tamaa za mwili, kama Samaria ilivyokuwa, je! lingempokea maskini jamaa huyu asiye na kadi ya ushirika, hakuna mtu wa kumdhamini, au wa kumsaidia kitu cho chote? Hakuwa na ufadhili. Hakuna kadi yo yote ya ushirika, hana shule aliyosoma. Lakini alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Na kuja Kwake, kama nabii, kulikuwa ni ishara. Yeye alikuwa sauti kutoka kwa Mungu, nayo ilitambulishwa katika siku za Yeroboamu wa Pili. Kila kitu alichosema kilitimia.

139 Sasa tunaona, siku hii tunayoishi, ni marudio tu ya mambo hayo tena. Wahudumu na watu, wanaona aibu kusimama mimbarani, na I—Injili inakuwa ni tikiti ya kununulia mlo. Wanaogopa kusema jambo lo lote, mtu fulani atawafukuza kutoka katika *hili*, *lile*, ama *linginelo*.

140 Kuna Mtu mmoja tu anayeweza kukufukuza Mbinguni, huyo ni Mungu. Nawe utafukuzwaje Mbinguni, ukidumu na Neno Lake? Hiyo ndiyo sababu ya Yeye kukutuma.

141 Kumbukeni, Biblia ilisema, katika wakati kama huo kama ilivyokuwa katika siku za Eliya, katika siku kama ilivyokuwa katika siku za Yohana, ya kwamba Malaki 4 itarudi duniani tena. "Nitawapelekea Eliya."

142 Sasa usichanganye jambo hilo basi na Malaki 3, "Namtuma mjumbe Wangu mbele za uso Wangu." Huyo alikuwa ni Eliya, pia.

143 Lakini katika Malaki 4, Yeye alisema, "Kabla tu haijaja ile Siku ya Bwana, iliyo kuu na ya kuogofya, wakati ulimwengu mzima utakapoungua kama tanuru, na wenye haki watatembea juu ya majivu ya watenda maovu," hiyo ni ule Utawala wa Miaka Elfu, "Nitawapelekea Eliya nabii." Naye atafanya nini? "Atairejeza imani ya watoto iwarudie baba wa kimitume," kurudi kwenye Neno. Itabidi awe ni nabii. "Nitampeleka." Yeye atatambulishwa kinaganaga kabisa. Tabia yake itakuwa kama ya Eliya ilivyokuwa, hasa. Ujumbe wake utakuwa wa jinsi hiyo kabisa. Atakemea, atararua-rarua. Hakuna ushirika, hakuna ushirikiano, hakuna cha nini, lakini atakuwa na BWANA ASEMA HIVI.

144 Sasa, kumbukeni, kumekuwako na kila namna ya vikundi vilivyoinuka na kusema, "*Hili* ni joho la Eliya, na *hili* ni fundisho la Eliya." Kundi zima, madhehebu, yanageuka na kuwa kundi la Eliya, ama joho la Eliya. Hayo si Maandiko. Mungu kamwe hajashughulika na kundi kama hilo.

145 Eliya alipojitokeza jukwaani, na Yohana Mbatisti, wote wawili walikemea vikundi hivyo na madhehebu hayo. Hawakufanya hivyo kamwe. Yeye anawakemea, kama

walivyofanya; Eliya na Yohana, wote wawili. Si kundi fulani wala madhehebu fulani. Lakini wote wawili, katika nyakati zao zote mbili, walikemea vikundi hivyo pamoja na madhehebu.

146 Ni nini basi? Ishara ya wakati wa mwisho hakika itaambatana na Sauti ya wakati wa mwisho. Eliya anapaswa aingie jukwaani, mtu aliyetiwa mafuta na roho hiyo; mtu apendaye kuishi mwituni, na kadhalika, na anayependa hayo, na ajitokeze jukwaani kusudi apate kuthibitishwa. Sasa angalia yale ambayo Maandiko yanena sasa, na ndipo hutadanganyika, unaona, ishara ya wakati wa mwisho na Sauti ya wakati wa mwisho.

147 Mungu kamwe hakujishughulisha na kundi, hakuna mahali po pote katika Maandiko. Yeye hujishughulisha na mtu mmoja binafsi, kwa maana kila mtu yuko tofauti na mwingine. Kila mtu, vidole gumba vyetu vinatofautiana, pua zetu ni tofauti, matendo yetu ni tofauti. Yeye anampata mtu mmoja, anaweza kumtuni kikamilifu mpaka anaweza kufanyika hilo Neno.

148 Hiyo ndiyo sababu Paulo, yeye alisema, "Nisije nikajiivuna juu ya wingi wa mafunuo, nilitumiwa mjumbe wa Shetani." Unaona? Mathayo aliandika, Luka akaandika, Marko akaandika, wote hao, bali, wao walimfuata Yesu tu na kuandika aliyosema. Lakini Paulo alipata ufunuo wa kwamba Yeye ni Nani, unaona, hilo ndilo jambo ali—aliloona. Ufunuo wake ulikuwa ni mkubwa sana, alimruhusu kuandika Biblia, kama vile Musa wa Agano la Kale. Yule mtu mashuhuri, Paulo, huo ufunuo aliokuwa nao, yeye alijua ya kwamba Yesu wa Agano Jipya alikuwa ndiye Yehova wa la Kale. Alikuwa na ufunuo wa jambo Hilo, naye angeweza kuuhubiri kwa Waebrania, kwa ninii. . .na pia kwa—kwa Warumi, na kwa Waefeso, na—na kwa wote. Yeye—yeye aliandika nyaraka hizi. Angalia, baada ya ishara yake kutokea, ndipo akaandika hizo nyaraka.

149 Tabia hii ya kule kuja itakuwa ni ile ile. Haitakuwa ni kundi fulani. Itakuwa ni mtu mmoja. Mungu kamwe hajawahi kutenda kazi kwa njia nyingine yo yote ila kwa mtu mmoja. Sasa, Eliya hakuwa ni kundi, Yohana Mbatizaji hakuwa ni kundi, walikuwa ni mtu mmoja mmoja. Mungu, Malaki 4, haisemi, "Nitapeleka kundi fulani." Alisema, "Nitampeleka Eliya!" Neno haliwezi kubadilishwa.

150 Sasa, angalia, ishara ya wakati wa mwisho na Sauti zitakuja kulingana na utaratibu wa Maandiko kama vile ilivyoahidiwa.

151 Tunataka kujua ishara ya mwisho itakuwa ni nini? Yesu alitwambia, katika Mathayo 24 na 25. Alitwambia, pia, katika Ufunuo, kote kote kutoka wa 6. . .ama wa 1, moja kwa moja mpaka, vema, mlango wa 10. Halafu Yeye anakuja katika mlango wa 19, ule Utawala wa Miaka Elfu unaanza katika wakati wa kuja Kwake, akiwa amepanda farasi mweupe.

152 Itakuja, ile ishara ya wakati wa mwisho. Sasa sikilizeni, katika kufunga. Itakuja kulingana kabisa na jinsi Maandiko yasemavyo. Sasa angalia ile Sauti ya ishara.

153 Sasa, Yesu, katika Luka 17:30, aliahidi ishara ya wakati wa mwisho. Ishara ya mwisho, ilikuwa ni Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu ambao ungeweza kutambua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara, katika hema nyuma yake. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Hiyo ndiyo ishara ambayo Yeye aliahidi wakati wa mwisho. Ka-. . . Ungesema ingefanya kitu gani? “Ingejulikana katika siku hizo, siku za mwisho, wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.” Atakapofunuliwa! Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa, hiyo ndiyo ishara atakayofunuliwa kwayo. Sasa angalieni kama Hilo halisemi hivyo. Bila shaka linasema.

154 Sasa ungeweza kusema, ya kwamba, “La, itakuwa ni jambo lingine. La, itakuwa ni kujenga jengo kubwa, nini *hii* kubwa, ama *hii*, ama baraza fulani kuu la ekumeni, ama cho chote kile”? Lo, la. La, huko ni kwenda mbali sana. Huo ni upande ule mwingine. Ni kinyume na yale Mungu aliyosema yafanywe, Yeye angefanya.

155 Angalia kile tulichosema sasa. Maandiko yatakuwa yanalingana vile vile kabisa, maana tuna ishara ya Sodoma, katika hali ya kimwili. Ni lini kulikuwako na walawiti wengi zaidi, upotovu na kadhalika, kama ilivyo sasa, “kizazi kiovu na cha zinaa,” wakati ambapo hata huwezi kufungua televisheni yako pasipokuwapo na aina fulani ya upuuzi mchafu, mbaya sana wa Hollywood? Na watu, wanaojiita Wakristo, watakaa nyumbani wasiende kwenye mikutano ya maombi ili waangalie vitu kama hivyo. Inaonesha una roho wa aina gani. Kweli. Na wanawake watavaa tu kama hao, na wanaume watawaacha wawaongoze huku na huko kama wanavyofanya kule. Je! tutafanya Hollywood kuwa ndio mfano wetu, ama tutaliamini Neno la Mungu kuhusu jambo hilo?

156 Na kundi lilo hilo linaweza kuona Neno la Mungu likithibitishwa, nao watafanya nini? Wanalicheka. Kwa sababu, wamekufa, wamekufa Milele. Hawajawahi kamwe kuwa hai. Kama walipata kuwa hai, wengekuwa hai sikuzote, Milele. Bali hawajawahi kamwe kuwa hai. Walikuwa sikuzote wamekufa. Loo, huenda wakawa wameng’arishwa, na kuamini *hili*, *lile*, ama *linginelo*.

157 Yesu aliwaambia, “Enyi wanafiki,” hao, hao makuhani katika siku hiyo. “Mnawezaje kunena mambo mema, ambapo kinywa cha mtu hunena yaujazayo moyo wake? Kuniita Mimi mwema, ‘Mwalimu mwema, Bwana mwema’?” Alijua yaliyokuwa moyoni mwao. Aliweza kutambua kilichokuwa moyoni mwao. Yeye alikuwa ndio lile Neno.

158 Biblia ilisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo yaliyo moyoni."

159 Sasa, ishara hiyo ya Sodoma imerudi, katika hali ya kawaida. Na kama kila kitu kimekaa barabara kwenye nafasi yake jinsi kinavyopaswa kuwa katika maumbile ya kawaida, basi unawezaje kuliondoa, mawazoni mwako, ya kwamba ya kiroho nayo hayako papa hapa wakati huu huu? Picha zote mbili zimejitokeza jukwaani. Naam, kila mtu anakubali, ya kawaida ni dhahilri; lakini, loo, kiroho, wao hawataki kuamini jambo hilo, kwa kuwa linaingilia fundisho lao.

160 Luka 17 ndiyo hiyo ishara. Luka 17 ndiyo ishara ambayo Yesu alisema, kwamba, katika siku za mwisho, nchi na makanisa na watu wangekuwa kama tu ilivyokuwa Sodoma, Yaani ulimwengu wa Mataifa, kabla tu ya kule kuteketezwa kwa Sodoma kwa moto. Na kutakuwako na kundi, likiangalia, kama Ibrahimu. Rejeeni, wakati Yesu aliposema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," rudini nyuma na mwone jinsi ilivyokuwa kule Sodoma. Yeye alisoma Biblia hii hii tunayosoma sisi, Biblia hii hii, sasa rudini nyuma mwone ilivyokuwa.

161 Hapa palikuwako na kundi teule, lililoitwa litoke, kundi la Ibrahimu, walikuwa wakimtazamia mwana wa ahadi. Wasodoma hawakuamini kitu cho chote kuhusu hilo. Na kulikuwako na lile la vuguvugu, mshiriki wa kanisa kule Sodoma. Angalia wale Malaika watatu wakija kwa kila moja la hayo, angalia zile ishara walizoonesha, ndipo utaona tunaishi katika ishara gani.

162 Basi, hiyo itakuwa ndiyo hiyo ishara. Na sauti ya ishara hiyo itakuwa ni Malaki 4, "kuwarejeza watu kwenye Imani ya mitume ya baba zao." Hiyo hapo ile ishara, hiyo hapo ile Sauti, kulingana kabisa na Maandiko. Unaona? Ishara hiyo ndiyo ile ishara iliyokuwa huko Sodoma, Mungu akidhihirishwa katika wanadamu.

Basi Yeye akasema, "Yuko wapi mkeo, Sara?"

Kasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

163 Kasema, "Nitakuzuru kulingana na wakati niliokuahidi." Basi akasema . . .

164 Naye Sara, huko nyuma, nyuma Yake, akasema, "Hilo lingewezekanaje, mimi bibi kizee, naye ni mwanamume mzee? Na kama vile mume wangu huko nje, mzee," kasema, "hatufanyi mambo kama hayo sisi." Kasema, "Haiwezekani kabisa."

165 Akasema, "Kwa nini Sara akatilia shaka jambo hilo, akisema moyoni mwake, 'Mambo haya yanawezekanaje?'"

166 Na Yesu alisema jambo hilo litarudi tena. Sasa, kumbukeni, Ibrahimu alimwita Mtu huyo, "Elohimu," Mungu. Ingebidi awe ni Mungu. Kwa nini? Yeye angeweza kutambua mawazo, Naye alikuwa katika wakati kikamilifu. Na Elohimu, Roho

Mtakatifu, (si mtu mwingine) Mtu yuyo huyo akirudi kanisani na angefanya jambo lile lile, hiyo ingekuwa ndiyo ishara. Nayo Sauti ingekuwa, "Waite warudi kwenye Neno, kuirudisha Imani ya watoto iwarudie baba zao." Hiyo hapo ile ishara na ile Sauti.

167 Ishara kwa kawaida hukubaliwa, lakini Sauti haikubaliwi. Watu hawaitaki hiyo Sauti, bali wataichukua hiyo ishara. Kwa kawaida, wataichukua. Wao wanapenda ishara, maana wanapenda kuiangalia, inawafurahisha. Lakini, ile Sauti, wao hawataki ku—kuikubali. Kumbukeni sasa ile sauti.

168 Rudini kwenye Neno tena. Ishara ya Yesu ya Masihi, kulingana na Isaya 35, "Viwete wataruka kama ayala," na yote haya.

169 "Hilo lilikuwa ni la ajabu sana!" Loo, hilo walilikubali. Hilo lilikuwa linafurahisha. Waliamini jambo hilo. Waliamini ile ishara. "Karibu, Rabi, kanisani mwangu, tutakuunga mkono kikamilifu. Hakika, tunakuamini. Wewe ni wa ajabu sana. Wewe ndiye Rabi yule. Wewe ni Nabii kijana. Karibu! Kila namna ya ushirikiano! Ishara hiyo ni nzuri sana."

170 Lakini wakati ile Sauti iliponena, na kusema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja."

171 Loo, jamani, hawakuweza kuamini jambo Hilo. "Wewe unajifanya Mwenyewe u Mungu." Hawakuitaka hiyo Sauti. Ishara waliitaka. Wanaijua, walikubali ilikuwa ni ishara ya Masihi, lakini, ile Sauti, hawakuitaka Hiyo.

"Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

Nao wakasema, "Yeye ni Beelzebuli."

Akasema, "Enyi uzao wa nyoka."

172 Loo, walichukia Sauti hiyo. Walifanya nini? Waliiondoa hiyo Sauti kati yao. Wakamfukuza.

173 Yesu alisema, "Kama wakimwita Bwana wa nyumba, 'Beelzebuli,' ni zaidi sana jinsi gani watawaita wanafunzi Wake?"

174 Kumbukeni, katika Ufunuo 3, kwenye wakati wa Laodikia. Huu ndio wa Laodikia; ile ishara ya Sodoma itakuja. Ile Sauti, "Rudini kwenye Neno, achaneni na kanuni hizi za imani na madhehebu, na mkaligeukie Neno," wakati Hiyo itakapokuja, kulingana na Ufunuo 3, Yeye alitupwa nje ya kanisa, kama tu alivyofanyiwa wakati huo.

175 "Ishara hiyo ni sawa, bali si Sauti." Hawataki uhusiano wo wote na Sauti hiyo. La, la; ile Sauti. Lakini Musa alisema, kama hawata-, ama . . .

176 Mungu alimwambia Musa, "Wasiposikia sauti ya kwanza ya ishara ya kwanza, wajaribu kwa sauti ya pili. Na endapo hawatafanya hivyo, basi nenda ukachukue maji kidogo ukayamwage juu ya nchi." Hilo linatosha. Ni hivyo tu.

"Nawa, ma—mavumbi kutoka miguuni mwako," kwa maneno mengine, kama alivyosema Yesu. Kasema, "Chota maji mtoni, yamwage ardhini, yatakuwa damu, na uoneshe ya kwamba hayo ndiyo yatakayowagharikisha, damu." Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa.

177 Kama hawakuamini ishara hiyo, basi ile ishara ya tatu kweli iliwapata. Huduma zote zina ishara tatu, kama zimetumwa kutoka kwa Mungu. Yesu alikuwa na ishara tatu. Musa alikuwa na ishara tatu. Nuhu alikuwa na ishara tatu. Eliya alikuwa na ishara tatu. Kila kitu kinakuja katika ishara tatu. Angalia. Sikilizeni, enyi marafiki.

178 Muda umeenda kidogo. Ninaninii. . . Loo, jamani, sikujua ulikuwa imeenda hivyo, imepita robo.

179 Kama unaweza kuamini ishara ya Sodoma, ya Luka, unaona, kama alivyoiahidi; ukiamini ishara ya Sodoma, basi kwa nini huwezi kukubali ile Sauti ya Malaki inayofuata ishara hiyo, "kurudi kwenye Neno"? [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] Biblia inasema hivyo, nawe unaona hilo, basi sikiliza ile Sauti ya hiyo ishara.

180 Ikimbieni hasira ijayo! Usifikiri, "Kwa sababu mimi ni mfuasi wa UPC, Assemblies of God, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, nina haki ya kuingia." Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Ligeukieni Neno! Ondokeni kwenye malimwengu yenu na mifumo yenu ya madhehebu, na kadhalika. Mungu ataiangamiza toka katika uso wa nchi. Atayazamisha katika vilindi vya bahari ya usahaulifu, kama tu vile alivyoifanyia Misri wakati alipowaita Israeli, taifa kutoka katika taifa. Wakati anapomwita Bibi-arusi kutoka katika kanisa, yeye atapitia kwenye zile dhiki, ailoweshe nchi kwa damu yake. Ikimbieni hasira ijayo, kwa kuwa imekaribia!

181 Hamwezi kuona mambo haya bila . . . Sijui mnafikiri nini juu ya hayo. Mimi ninahusika tu na kuyasoma na kuzungumza juu yake. Ni juu yako! Kama unaweza kuiamini ile ishara, basi amini hiyo Sauti inayoifuata ishara hiyo. Loo, jamani!

182 Angalia, Musa, ule mfano wa kutoka sasa. Alikuwa awaambie watu hao juu ya ahadi iliyotolewa kwa baba zao. "Ninakumbuka ahadi Yangu kwa baba zao." Na sasa Musa atafanya—atafanya nini? Kuigeuza mioyo ya watu hao ielekee kwenye yale baba zao waliyokuwa wamesema. Na kama vile Musa alivyokuwa wakati huo, vivyo hivyo na Malaki 4, "kuwageuza watu waelekee kwenye Imani ya baba zao."

183 Aibu hii yote ya madhehebu, na kadhalika, rudini kwenye Neno! Ninajua ninyi, watu wengi wanapenda kufanya jambo hilo; mimi siwakemei tu hapa. Kanda hizi husambazwa ulimwenguni kote, unaona, kila mahali. Mimi siwakemei ninyi, lakini ninamkemea mtu ye yote yule, po pote panapohusika.

Mimi ni mpanzi wa mbegu. Hivyo tu ndivyo ninavyojua kufanya. Ni juu yenu kujiamulia. Ikimbieni hasira ijayo, enyi watu!

184 Usifikiri ati kwa sababu wewe ni Mpentekoste. Usifikiri ati kwa sababu mama yako alikuwa Mmethodisti mzuri, aliyetakaswa, ama baba yako Mbaptisti mzuri, mwenye kupiga makelele. Usifikiri ya kwamba jambo hilo litakuwa na uhusiano wo wote nawe. Usifikiri ati kwa sababu wewe ni mfuasi wa kanisa walilojenga, ama kanisa ambalo mnalijenga sasa. Usifikiri ati kwa sababu ninyi Wapentekoste mlinena kwa lugha na kucheza katika Roho, na kukimbia huku na huku sakafuni, miaka arobaini iliyopita. Usifikiri ati kwa sababu mlikuwa na mikutano ya uponyaji, na kadhalika.

185 Usishindwe kuona hiyo ishara, ya Nguzo ya Moto, ambayo Mungu amethibitisha; na Sauti iliyo nyuma Yake, kumgeukia, kumrudia Mungu. Usiache Hiyo ikupite. Hiyo hapo ishara na Sauti.

186 Mtu anapoinuka akiwa na ishara, itikadi ile ile ya kale, kuna kasoro fulani, haitoki kwa Mungu. Loo, jamani! "Yanyosheni mapito Yake sasa!" Sasa, mnaamini jambo hilo? "Basi rudini, Enyi vipofu na mliotawanyika, makwenu." Biblia . . . Mwandishi wa wimbo alisema:

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
> Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
>   na hofu;
> "Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

187 Rudini! Rudini! Nabii alisema, "Kutakuwako Nuru wakati wa jioni." Kabla tu Mwana hajaondoka, kutakuwa Nuru. Tembea katika Nuru wakati kuna Nuru. Baada ya kitambo kidogo Baraza la Ekumeni litakupata, na hakutakuwa na njia ya Nuru wakati huo.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

188 Baba wa Mbinguni, liko mikononi Mwako sasa. Ni— nilipanda Mbegu. Sijui zilikoangukia. Ninaomba kwamba utazibariki po pote zilipo. Na jalia zipate mahali Pao huko chini kabisa, na ziondolee mbali mahali pote penye mawe, na mashina yote ya majani mabichi ya michongoma, na kama ilivyokuwa, na uondolee mbali kutokuamini kote. Tujalie, Baba. Tunakabidhi jambo hili sasa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

189 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, macho yenu yamefungwa. Kesho usiku kuna karamu. Wenye dhambi wa jiji hili, nitaninii . . . Bwana akipenda, itanibidi kuzungumza nao. Ninazungumzia kusanyiko lililochanganyikana sasa. Nisingethubutu kuhubiri jambo hili; lingewafanya tu kuwa vipofu zaidi kuliko walivyowahi kuwa, kwenye mkutano kama huo.

190 Lakini, wewe, usiku wa leo, je! unaamini ya kwamba umeiona ile ishara, na je! unaweza kuisikia ile Sauti, kama umeisikia na je! unaiamini? Na hu—hujaninii, unaamini lakini bado hujaikubali bado, Kristo katika utimilifu Wake, je! ungeinua mkono wako? Na hebu kila kichwa kiinamishwe sasa, na kila jicho lifumbwe. Inua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba." Nitafurahia kufanya hivyo. Mungu awabariki.

191 Baba yetu wa Mbinguni, Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa." Ninaomba, Bwana, ya kwamba watu hawa ambao wameinua mikono yao, ya kwamba wanaamini jambo hilo. Wao hawajabatizwa katika ubatizo wa Kikristo, jalia wapate kanisa linalofanya jambo hilo, na wakabatizwe. Tujalie, Bwana.

192 Jalia kwamba wasibatizwe tu kwa maji, ambayo ni ishara ya nje ya kwamba jambo fulani ndani limetendeka. Biblia ilisema, "Kuna Imani moja, Bwana mmoja, ubatizo mmoja," na ubatizo huo ni ubatizo wa kiroho. Wakati mwili unapooshwa, ni mfano tu, ama kutoa ishara ya kwamba jambo fulani ndani limetendeka. Lakini ni hiyo nafsi ndiyo inayopaswa kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, huyo ni yule wa Milele akiingia katika tabia ya mwanadamu na kuibadilisha, na kuifanya kuwa mwamini. Ninaomba ya kwamba wao watampokea Roho Mtakatifu. Ninawakabidhi Kwako sasa, kama tunzo la Ujumbe, na la Neema ya Kristo. Katika Jina Lake, ninaomba. Amina.

Sasa huku mmeinamisha vichwa vyenu, kwa uchaji.

193 Nina dakika saba tu, ni—nisingeweza kutoka nje kwa wakati mzuri. Ni—ni—nisingeweza kufanya mstari wa maombi katika muda wa kiasi hicho. Nitawaomba mketi mahali tu mlipo. Ninasikitika kwa kuwachelewesha. Tutamwombea kila mtu. Ninyi watu, baadhi yenu hapa walio na kadi za maombi, msijali, tutawafikia.

194 Lakini tutaona tu kama Roho Mtakatifu atatufunulia sasa, kama mnamwamini na mnaamini ya kwamba hii ndiyo ile ishara. Kumbukeni, yule Malaika, Yeye alikuwa ni mwanadamu; alikula, alikunywa mbele za Ibrahimu, na hata hivyo Yeye aliweza, na Sara akiwa hemani, angeweza kutambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwake. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara. Yeye alikuwa Neno. Sasa kama Neno lingaliweza tu kutujia sisi, basi, pia, Yeye aliahidi kufanya jambo lile lile.

195 Sasa ninyi mlio huko nje kwa wasikilizaji, ambao hamna kadi za maombi, nanyi mnajua hamtakuwa katika mstari, siwezi kuwatambua nani ni nani isipokuwa Bwana aonioneshe. Nitaninii. . .Nanyi mnaamini ya kwamba Mungu hakika huwaponya wagonjwa. Ni—ninawatakeni mwa—mwamini sasa hivi, kwa dakika chache. Na mwombe tu, na kusema, "Bwana Yesu, ninamjua mtu huyu, anayenena, ni—ni mwanadamu, bali yeye aliniambia jambo hilo, ametuambia usiku wa leo,

na kututhibitishia; ya kwamba, Roho Mtakatifu, ya kwamba ulimwengu hauwezi kumwua."

196 Waliweza kumwua Yesu alipokuwa katika mwili; walimwua. Lakini sasa Yeye amefufuliwa, katika hali ya utukufu, hawezi kuuwawa tena. Naye alisema, "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi," mliochaguliwa tangu zamani, wale mliokusudiwa kwa ajili ya Uzima wa Milele, Kanisa, Bibi-arusi, "mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Mambo nifanyayo mimi, ninyi nanyi mtayafanya." Ahadi hizi zote alizofanya.

197 Sasa, ninajua wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye, Mungu, alikuwa ndani Yake. Yeye alikuwa ni Mungu. Yeye alikuwa utimilifu wa Mungu. Alikuwa ni Neno lote la Mungu lililodhihirishwa.

198 Na Biblia ingali ni Mungu, lile Neno, na bado kuna ufunuo mwingine zaidi utakaofunuliwa. Naye alisema, "Katika siku za mwisho, wakati ulimwengu utakapokuwa katika hali ya Sodoma tena, Mwana wa Adamu atafunuliwa." Na ile ishara ya Sodoma itarudi, ndipo ile Sauti itawaita watu warudi, hao waliochaguliwa kwa Uzima wa Milele.

199 Tunajua, wakati Yeye alipokuwa hapa, kulikuwako na mamilioni ya watu duniani, ambao hawakujua kamwe Yeye alikuwa yupo hapa; hawakuwa na sababu ya kujua. Unaona? Yeye alikuja kwa wale waliochaguliwa tangu zamani kuliona.

200 Sasa ninyi ombeni. Sasa iweni kimya kabisa. Msisogee. Po pote mlipo, roshani, kwenye orofa za chini, po pote mlipo, msi—msisogee, ketini kwa utulivu kabisa.

201 Na mwombe, mseme, "Bwana Yesu, Biblia ilisema, katika Waebrania 4, ya kwamba Wewe sasa hivi ni 'Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana na sisi katika mambo yetu ya udhaifu.' Nasi tunakuona duniani, wakati ulipokuwa hapa duniani, maskini mwanamke mmoja wakati mmoja aligusa vazi Lako, nawe ukageuka, na kusema, 'Ni nani aliyenigusa?'" Akajificha, lakini hata hivyo imani yake ilitambulishwa. Yesu alimwambia kuhusu kuvuja kwake kwa damu, na akasema imani yako "imekuokoa." Sasa Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, itambidi kutenda vile vile, kama u—kama ukimgusa.

202 Na jambo hilo linafanya nini basi? Hapana budi kuweko na mwili wa kibinadamu duniani, kunena kwa Sauti Yake. "Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi." Hakuna njia ya kuepa jambo hili, enyi marafiki. Ni Maandiko tu. Ni Kweli. Ninyi wahudumu mnaamini jambo hilo, kule nyuma? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.]

203 Sasa huko nje, iweni na kicho tu sana na mwombe, mseme, "Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako."

204 Nanyi mnaona aliye karibu sana nami, yuko futi ishirini ama zaidi. Mimi sijui mtu ye yote huko nje. Hata siwezi kuona mtu ambaye kwa kweli ninamjua, usiku wa leo, aliyeketi pale; ila Pat Tyler anayeketi hapa mbele, rafiki yangu. Kuna watu kwenye vitanda vya wagonjwa, machela.

205 Tuliona machela ikifunguliwa jana usiku, naye mtu huyo akasimama akaenda zake. Mbona ninyi nyote msifanye hivyo, usiku wa leo? Unaona, amini tu, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya. Uwepo Wake utafanya jambo hilo. Huyu hapa, itakubidi kusimama karibu Naye apate kukuinua katika siku za mwisho.

206 Sasa, ninyi mnaoamini, na mnafikiri mnaomba vizuri, hebu angalieni tu upande huu sasa.

207 Kama vile Petro na Yohana walivyosema, "Tuangalie." Nao wakaangalia kwa moyo, mtu huyo aliangalia kwa bidii, akitarajia kuona jambo fulani. Akasema, "Fedha na dhahabu sina, lakini nilicho nacho . . . "

208 Sasa, uponyaji sina, lakini nilicho nacho, karama kutoka kwa Mungu, nakupa. Kama tu utaamini, Mungu ataitendea kazi. Ninakuomba tu uiamini. Nilicho nacho, nitakupa. Kama utaamini, Mungu atatenda kazi. Hebu jaribu tu.

209 Amewasili, Huyu hapa sasa hivi. Amina. Ninapenda jambo hilo. Kuna mama fulani anayeketi papa hapa. Yeye ni mnene hivi, ameketi papa hapa mwishoni. Je! una kadi ya maombi, mama? Mnene hivi . . . Huna ninii . . . Papa hapa, huna kadi ya maombi? Naam. Ati huna kadi ya maombi? Unaamini, hata hivyo? Huhitaji kadi ya maombi, kama unaamini.

210 Kuna kurudishwa nyuma kwa sauti, hiyo ndiyo sababu ni vigumu kuwaita watu namna hii, lakini jaribuni kunisikiliza kwa makini mwezavyo sasa.

211 Mimi sikujui. Huna kadi ya maombi, kwa hiyo hutakuwapo jukwaani. Kama Mungu atanifunulia mimi shida yako ni nini, utaamini ya kwamba (ati nini?) ingekuwa ni jambo lile lile kama tu vile alivyomfunulia yule mwanamke kwamba shida yake ilikuwa ni nini? Yule mwanamke pale kisimani? Sara, yale aliyokuwa amesema, na kadhalika? Je! unaamini jambo hilo? Je! unaamini hilo lingekuwa ni sawa?

212 Unaugua ugonjwa wa damu, kuna kasoro na damu yako. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Huna kasoro hiyo sasa. Inageuka kuwa Nuru juu yako. Yesu Kristo amekutunukia.

213 Sasa, sijawahi kumwona mwanamke huyo, maishani mwangu. Sasa hicho ni kitu gani? Haina budi kuwa ni roho. Sasa unaweza kusema kama Mafarisayo, "Huyo ni ibilisi," vema, unapata thawabu yao. Ukisema, "Ni Kristo," unapata thawabu

ya Kristo. Mimi ninaamini ni Neno likitambulishwa katika siku hizi za mwisho; si mimi.

214 Hapa, huyu hapa maskini bibi mwingine anayeketi chini papa hapa. Anateseka na amevimba mishipa ya damu ya miguu yake. Ana matatizo chungu nzima. Ana shida ya moyo. Anamwombea mpendwa wake, huyo ni kaka yake. Analia sasa. Amegusa. Ndugu huyo ni mahututi sana. Ni ugonjwa wa kisukari. Na, pia, ana kivuli kingine, yeye ni mwenye dhambi. Nawe unamwombea. Hiyo ni kweli. Bibi Welton, kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atamfanyia jambo hilo. Unaamini? Hilo ndilo jina lako. Unaona?

215 Sasa je! hiyo ni zaidi ya vile Yesu alivyomwambia Simoni, "Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona"? Iweni na imani tu. Msitilie shaka. Aminini kwa mioyo yenu yote. Kama ukiamini jambo hilo, Mungu atalitimiza. Kama unaweza tu . . .

216 Naam, huyu hapa maskini bibi mmoja ameketi hapa, akiniangalia moja kwa moja hapa. Ana nywele nyekundu hivi. Nywele zake zimelazwa nyuma.

217 Je! hamwezi kuona ile Nuru, ya rangi ya kaharabu hivi, ikizunguka-zunguka juu ya yule mwanamke? Yeye anajua jambo hilo linatukia sasa hivi, maana anaihisi. Iko karibu sana naye, hawezi kujizuia kuisikia. Kama hiyo ni kweli, bibi, inua mkono wako. Huyo hapo.

218 Sasa mimi ni mgeni kabisa kwako. Sijui lo lote kukuhusu wewe. Lakini ulikuwa umeketi pale ukiomba. Hiyo ni kweli. Kama hilo ni kweli, tikisa mkono wako namna *hii*. Sasa, kama Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na Ndivyo alivyo, Kuhani Mkuu anayeketi mkono wa kuume wa Mungu . . . Nami ninasimama hapa tu kwa karama fulani, mimi mwenyewe nikiwa ninii . . . nikiwa nje, nje tu ya mawazo ya kibinadamu, bila kufikiria kwa nafsi yangu; njia ya kutuliza moyo wangu na mawazo, na kumwacha tu Mungu aingie ndani. Je! unaamini ya kwamba Yeye . . . Mimi, Mungu anajua mimi sikujui wewe; nawe unajua vivyo hivyo. Kwa hiyo kama Mungu atanifunulia mimi shida yako, ama jambo fulani unalongojea, unalotaka, ama jambo fulani zaidi, je! unaamini ya kwamba Mungu atafanya ninii, anaweza kufanya hayo?

219 Una shida ya mgongo wako. Hayo ni moja ya mambo unayoombea. Pia una shida na macho yako. Unaamini ya kwamba Mungu atayaponya na kuyafanya mazima? Unaamini? Unaamini? Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Hallman, amini sasa kwa moyo wako wote waweza kupokea, uliyoomba. Unaamini?

220 Huyu hapa mwanamke mzee anayeketi mbali kidogo nyuma yake kule. Anaomba, pia. Ana kisukari. Ninatumaini hatakosa jambo hili. Iko moja kwa moja juu yake. Yeye ni mzee kidogo. Hebu kidogo, Bwana na anisaidie sasa. Ninii yake . . . Hapo

amelipata, vema, sasa, unaona, wakati alipokuwa anawasiliana. Yeye hatoki hapa. Anatoka Louisiana. Ji—jiji lake ni mahali panapoitwa Singer, Louisiana. Naye anaugua kisukari. Jina lake ni Bibi Doyle. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Mimi ni mgeni kabisa kwake, sijapata kumwona maishani mwangu. Lakini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anajua yote kukuhusu.

221 Kuna bibi anayeketi nyuma kule, kutoka mji huo huo, mahali panapoitwa Singer. Anaugua shinikizo la juu la damu. Na jina lake ni Clark. Unaamini, Bibi Clark? Vema, unaweza kupokea ulichoomba.

Unaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

222 Hiyo hapo hiyo ishara! Isikilizeni hiyo Sauti! Tubuni, rudini kwa Mungu upesi mwezavyo! Yesu Kristo yuko hapa katika nguvu za kufufuka Kwake; kizazi kiovu na cha zinaa kinapokea ishara ya Yesu Kristo akiishi miongoni mwa watu. Asingeweza kufanya jambo hilo na mimi tu, haina budi kuwa na wewe, pia. Unaona, ilibidi yule mwanamke aguse vazi Lake. Ilikubidi kugusa vazi Lake. Sisi ni vyombo tu.

223 Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa kama unaamini jambo hilo . . . Ni wangapi wanaliamini, inueni mikono yenu, namna *hii*, mkaseme, "Kwa kweli ninaamini."

224 Sasa kama unaamini jambo hilo, Yesu alisema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kama wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Unaamini jambo hilo?

225 Sasa muda umeenda. Hatuna wakati. Ni saa nne kasoro dakika ishirini na tano sasa. Basi, mtawekeana tu mikono ninyi kwa ninyi? Na mfanye tu ninavyowaambia sasa, wekeaneni tu mikono ninyi kwa ninyi.

226 Sasa mnajua, huko juu, po pote mlipo. Sasa mnajua, dhahiri kabisa sasa, baada ya Maandiko kuhubiriwa na kutambulishwa dhahiri kila mahali jengoni.

227 Ninaona mwingine, sasa hivi. Unaona? Na mwingine papa hapa, shida ya kibofu cha mkojo. Bibi fulani mwenye TB. A-ha. Loo, iko kila mahali sasa, lakini Hiyo inakudhoofisha.

228 Muone nini tena, muone nini zaidi? Mnaona hamsini, wakati mwingine kuna idadi hiyo, nanyi mnataka kuona sabini wakati ujao. Yesu alifanya hivyo wakati mmoja huko Sikari, na jiji zima likamwamini. Walikuwa wakimtarajia Masihi.

229 Masihi yuko hapa, Roho Mtakatifu, Masihi wa siku hii; Masihi anayefanya Neno lithibitishwe, la ahadi Yake.

230 Sasa nataka kila mmoja wenu, mnapowekeana mikono ninyi kwa ninyi, kama ninyi ni waamini. Sasa usijiombee. Wewe mwombee mtu huyo, nao watakuwa wanakuombea. Sasa, Neno lile lile lililoahidiwa katika siku za mwisho, liliahidi pia . . .

231 Pia kumbukeni, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kule kuponywa, kukirudi, ni sauti ya kwamba ile ishara imekubaliwa. Wanaweka mikono juu ya wagonjwa, kama ishara; ile sauti ni "haleluya, Bwana ameniponya!" Sasa kama ishara hizi zinaambatana na sauti, hiyo ishara, kama wewe ni mwamini, itaambatana. Hiyo sauti itaambatana na ile ishara.

232 Kama nikiwapa ishara hii, ambayo niliwaambia inatoka kwa Mungu, na Mungu aliiahidi katika siku hii ya mwisho; imeelezwa kinaganaga kabisa, hakuna kitu ila kafiri angeweza kutokuiamini. Unaona? Ndipo Mungu akageuka na kuithibitisha, kuifanya dhahiri. Sasa Yeye yuko hapa.

233 Sasa kila mmoja, kwa jinsi unavyoomba katika kanisa lako mwenyewe, kama ni kimoyomoyo, kwa sauti kuu, vyo vyote vile, wewe mwombee mtu ambaye uliyemwekea mikono, maana wao wanakuombea.

234 Na sasa angalieni juu. Na mbele ya Masihi, yule Kristo, Yeye Aliyefufuka, ambaye angali hai baada ya miaka elfu mbili, tunawezaje kuwa wazito hivi katika Roho? Hilo linapaswa kuchochea Moto taifa hili. Hilo linapaswa kuifanya Beaumont itubu, katika magunia na majivu. Lakini je! itafanya hivyo? La.

235 Lakini ninyi mnaomtazamia Yeye, na mnaamini ya kwamba angefanya jambo hilo na kutimiza Neno Lake, ninyi ndio sasa mmepewa ile ahadi. Weka mkono wako juu ya mtu fulani na uombe, ninapowaombea kutoka hapa.

236 Bwana Yesu, yamesemwa ya kutosha, yamefanywa ya kutosha. Neno lililoahidiwa limedhihirishwa. Yule Masihi, Kristo wa Mungu, yuko katika Uwepo wa Kiungu. Tunamhisi. Tunamwona. Tunajua ya kwamba aliahidi jambo hili katika siku za mwisho. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati atakapofunuliwa Mwana wa Adamu." Ndipo, tunajua.

237 Tunaona niniii—moto mbinguni, bomu za atomiki. Tunaona mataifa yaliyoliwa na funza, mataifa yakivunja. Tunaona ya kwamba Israeli iko katika nchi ya uenyeji wake. Kila ishara ambayo ingeweza kuahidiwa, imetimizwa. Jambo linalofuata ni Mwana aliyeahidiwa, Kuja.

238 Ee Mungu wa Milele, katika Uwepo wa Yesu Kristo, yule Roho Mtakatifu aliye mkuu ambaye yuko hapa sasa akithibitisha ya kwamba Yeye yuko hapa, yasikie maombi ya watu hawa, wasikie Wakristo hawa; ili kwamba, nitakapoondoka, hawatasema, "Ndugu Branham alifanya jambo hili." Mtu mwingine wasiyemjua, aliwawekea mikono, nao wakaponywa. Lakini Wewe umeahidi ya kwamba ile Sauti ilikuwa inafuatwa na ishara. Na jalia waponywe, ninapowakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu.

*SAUTI YA ISHARA* SWA64-0313
(The Voice Of The Sign)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, 13 Machi, 1964, katika Municipal Auditorium kule Beaumont, Texas, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org